

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO



TANGAZO LA MARUDIO

Tarehe 02/07/2021

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUTUMA MAOMBI YA KUPANGA VYUMBA
VYA BIASHARA KATIKA JENGO JIPYA LA KITEGA UCHUMI CHA DDC**

FURSA ZA KIBIASHARA ZILIZOPO

Na	Aina ya fursa	Idadi	Bei ya fomu
1	Upangishaji wa vyumba vya biashara	6	50,000.00

Malipo yote yatafanyika ofisi kuu Manispaa ya Morogoro mara tu baada mwombaji kupatiwa namba ya malipo (Control number), Fedha hizi hazitorejeshwa.

VIGezo KWA MUOMBAJI

- Nakala halali ya leseni ya biashara .
- Nakala ya kitambulisho cha Taifa , cha mpiga kura au leseni ya udereva.
- Picha mbili za pasipoti.
- Mwombaji awe na Mdhamini mmoja (mtumishi wa umma).
- Nakala ya cheti cha mlipa kodi (TIN NUMBER)
- Mwombaji awe tayari kufungua biashara ndani ya wiki moja baada kushinda zabuni hii.

NB: Wale waombaji wa awali ambao walishafanya malipo ya fomu, waje na risiti za malipo na watapewa fomu hizo bila kulipia tena.

Fomu za maombi zinapatikana katika ofisi ya Manunuzi (PMU) Manispaa ya Morogoro kuanzia Tarehe 02/07/2021 saa 01:30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri, siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu.

Siku ya mwisho ya kuwasilisha fomu za maombi ni tarehe 15, Julai 2021 saa 6.00 mchana siku ya Alhamis, fomu zitafunguliwa hadharani mara baada ya kufunga zoezi la kupokea fomu hizo, ufunguzi utafanyika mbele ya Wazabuni/ wawakilishi wao watakao hudhuria katika ufunguaji wa fomu utakao fanyika 15 Julai, 2021 saa 6.00 Mchana katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro

Mashariti mengine, namba ya vioski na mahali vilipo vitaelezwa katika Fomu ya maombi.

NB: Waheshimiwa Madiwani na Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Watumishi wa Ofisi ya Mkuu mkoa na Mkuu wa wilaya hawaruhusiwi kushiriki zabuni hii.

WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA.

Pilly Kitwana

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO**